# BODI YA KOROSHO TANZANIA

## MWONGOZO NA. 2 WA USIMAMIZI NA UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI WA MWAKA 2025/2026

TOLEO LA 8

*Umetolewa na:-*

*Bodi ya Korosho Tanzania*

*S. L. P. 533*

*MTWARA*

*SEPTEMBA, 2025*

YALIYOMO

UKURASA

1. UTANGULIZI ........................................ 1
1.1 Maelezo ya Awali ........................................ 1
1.2 Sifa za Mtaalamu wa Ubora katika ngazi ya Chama Cha Ushirika Cha Msingi .. 1
1.3 Sifa za Mtaalamu wa Ubora katika ghala la mnada ........................................ 1
2.0. UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI NGAZI YA MKULIMA ........................................ 3
2.1. Uvunaji Korosho Ghafi ........................................ 3
2.2. Uanikaji wa Korosho Ghafi ........................................ 3
2.3. Uchambuaji (Sorting) ........................................ 3
2.4. Kuhifadhi Korosho Ghafi ........................................ 4
3.0. UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI KATIKA NGAZI YA CHAMA CHA USHIRIKA CHA MSINGI ........................................ 5
4.0. UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI KATIKA GHALA LA MNADA ........................................ 6
4.1. Taratibu za Kuingiza Korosho Ghala la mnada ........................................ 6
4.2. Utaratibu wa Kuchukua Sampuli ........................................ 7
4.3. Vifaa Vinavyohitajika Katika Zoezi la Uhakiki Ubora ........................................ 8
4.4. Taratibu za Kupima Sampuli ........................................ 8
4.5. Taratibu za Kutoa Korosho Ghala la Mnada. ........................................ 10
4.6. Sifa za Ghala la Kuhifadhia Korosho ........................................ 11
4.8. Udhibiti Ubora wa Korosho Ghafi Ngazi ya Msafirishaji ........................................ 12
5.0. MAJUKUMU NA WAJIBU WA WADAU KATIKA KUSIMAMIA UBORA WAKOROSHO GHAFI ........................................ 14
5.1. Mkulima ........................................ 14
5.2. Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) ........................................ 14
5.3. Mtaalam wa Ubora ghala la mnada ........................................ 15
5.4. Mwendesha Ghala ........................................ 15
5.5. Wanunuzi wa Korosho Ghafi ........................................ 17
5.6. Wasafirishaji wa Korosho Ghafi ........................................ 17
5.7. Halmashauri ........................................ 18
5.8. Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) ........................................ 18
5.9. Bodi ya Usimamiziwa Stakabadhi za Ghala ........................................ 18
5.10. Bodi ya Korosho Tanzania ........................................ 19
6.0. UTATUZI WA MIGOGORO ........................................ 20
RANGI NA ALAMA ZA MAGUNIA YA KOROSHO GHAFI MSIMU WA 2025/2026 ........ 21

## TAFSIRI YA MAANA ZA MANENO YALIYOTUMIKA

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| **AMCOS** | Chama cha Ushirika cha Msingi. |
| **UNION** | Chama Kikuu cha Ushirika. |
| **Cutting test** | Kupima ubora wa Korosho-karanga (kernel) baada ya Korosho ghafi kukatwa. |
| **First in First Out (FIFO)** | Utoaji wa korosho kwa kuzingatia Korosho zitakazoanza kuingizwa ghalani ziwe za kwanza kutolewa ghalani. |
| **Ghala la Chama cha Msingi** | Ghala la kukusanyia Korosho za wakulima kwa ajili ya kuzipeleka katika ghala la mnada. |
| **Ghala la mnada** | Ghala lililokidhi sifa na vigezo kwa ajili ya kupokea Korosho za wakulima zinazosubiri kuuzwa kwa mnada. |
| **Kanuni** | Kanuni za Tasnia ya Korosho za mwaka 2010. |
| **LBS** | Kipimo cha uzito katika ratili. |
| **Loti/ Stake** | Fungu la Korosho zilizopo katika ghala la mnada zinazosubiri kuuzwa kwenye mnada. |
| **Mchanganuo Mauzo (catalogue) wa (Sales)** | Kijarida cha taarifa ya Korosho ghafi kinachooonesha namba ya stakabadhi, tarehe ya stakabadhi, mmiliki, kiasi, idadi ya magunia, ubora,loti, namba ya mnada na ghala la mnada. |
| **Mfumo wa stakabadhi za Ghala** | Mfumo wa soko ambapo Korosho huwekwa katika ghala na kutolewa stakabadhi ikionesha kiasi, ubora na daraja la Korosho kwa lengo la kusubiri kuuzwa' |
| **Mnunuzi** | Mfanyabiashara aliye na leseni ya ununuzi wa Korosho kutoka Bodi ya Korosho Tanzania katika msimu husika. |
| **Msafirishaji** | Msafirishaji wa Korosho kutoka ghala la AMCOS hadi ghala la mnada na kutoka ghala la mnada Kwenda ghala la mnunuzi/bandarini. |
| **Mtaalam wa Ubora** | Mtaalam aliyefuzu mafunzo ya uhakiki ubora wa Korosho kisha kupata cheti kutoka Bodi ya Korosho |

| | |
|---|---|
| | Tanzania na leseni iliyouhishwa na kuajiriwa na mwendesha ghala/Mnunuzi/Chama Kikuu cha Ushirika kwa ajili ya kuhakiki ubora wa Korosho zinazoingia na kutoka ghala la mnada au ghala la Chama cha Msingi. |
| **Mwendesha Ghala** | Mtu/kampuni aliyepata/iliyopewa leseni kutoka Bodi ya<br>Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kwa ajili ya upokeaji, utunzaji na utoaji wa Korosho ghafi kutoka katika ghala la mnada. |
| **Nut count"** | Idadi ya Korosho ghafi katika kilo moja ya Korosho. |
| **PDN (Produce DispatchNote)** | Hati ya kusafirisha Korosho ghafi ndani ya nchi |
| **Shelling out turn** | Kiasi cha Korosho-karanga zinazopatikana baada ya kubangua gunia la korosho ghafi lenye uzito wa kilo 80 na huwasilishwa (presented) kwa ratili. |
| **Sheria"** | Sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 ya mwaka 2009 |
| **TBS (Tanzania Bureau of Standards)** | Shirika la Viwango Tanzania |
| **Unyevu (w/w)** | Asilimia ya majimaji (unyevu) uliomo katika mzigo wa korosho' |
| **Kipima Unyevu (Moisture Meter)** | Kifaa cha kinachotumika kupima asilimia za unyevu kwenye korosho |
| **Mizani** | Kifaa cha kupima uzito wa korosho ghafi kabla ya kuhakiki ubora. |
| **WMA"** | Wakala wa Vipimo Tanzania |

## SEHEMU YA KWANZA

### 1. UTANGULIZI

#### 1.1 Maelezo ya Awali

Mwongozo huu umetolewa chini ya sheria Na. 18 ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2010 kifungu cha 59.

Mwongozo huu unatakiwa kusomwa sambamba na sheria ya tasnia ya korosho Na. 18 ya mwaka 2009 (sura ya 203 ya sheria za Tanzania) pamoja na kanuni zake za mwaka 2010 (Tangazo la serikali Na.420 la mwaka 2010). Atakayekiuka matakwa ya mwongozo huu atakuwa anatenda kosa hivyo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.

Mwongozo unatoa maelekezo juu ya taratibu za usimamizi na udhibiti ubora wa korosho ghafi wa mwaka 2025/2026. Bodi ya Korosho Tanzania imeandaa Mwongozo huu kuwezesha wadau mbalimbali kujua taratibu zitakazotumika katika kusimamia ubora wa korosho ghafi kwa msimu wa 2025/2026. Aidha majukumu ya kila mdau yanayopaswa kutekelezwa kuanzia ngazi ya mkulima hadi bandarini yameainishwa ndani ya Mwongozo huu.

#### 1.2 Sifa za Mtaalamu wa Ubora katika ngazi ya Chama Cha Ushirika Cha Msingi

Mtaalamu wa ubora katika ngazi ya chama cha Ushirika cha Msingi anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

- **1.2.1** Awe amepata mafunzo ya udarajishaji wa korosho ghafi na matumizi ya Vifaa vya ubora kutoka Bodi ya Korosho Tanzania kwa mwaka husika.
- **1.2.2** Awe mkulima mzoefu.
- **1.2.3** Awe mjumbe wa Bodi au mtendaji wa Chama cha Msingi cha Ushirika husika.

#### 1.3 Sifa za Mtaalamu wa Ubora katika ghala la mnada

Mtaalamu wa ubora atakayeajiriwa na mwendesha ghala anapaswa kuwa na sifa zifuatazo :-

1.3.1 Awe na elimu angalau ya astashahada ya kilimo/ Sayansi ya chakula na tekinolojia au taaluma nyingine yoyote inayoshabihiana na kilimo.

1.3.2 Awe amepata mafunzo ya uhakiki/udhibiti ubora wa korosho ghafi na cheti kutoka Bodi ya Korosho.

1.3.3 Iwapo atakuwa na uzoefu (sifa ya ziada) wa kufanya kazi katika misimu iliyotangulia awe na historia nzuri ya utendaji kazi, uaminifu na uadilifu kutoka kwa mwajiri wa awali.

1.3.4 Awe amehudhuria semina za maandalizi ya kuanza msimu husika.

1.3.5 Awe ameomba na kupata leseni ya kufanya kazi ya uhakiki ubora kutoka Bodi ya Korosho Tanzania baada ya kupata mkataba wa kazi kutoka kwa mwendesha ghala.

1.3.6 Mtu yeyote atakayegundulika kufanya kazi za uhakiki ubora ghala la mnada bila kuwa na sifa tajwa hapo juu na hajasajiliwa na Bodi ya Korosho Tanzania atawajibika kulipa faini shillingi milioni mbili (2,000,000/=) na asiendelee na kazi. Kwa mwendesha ghala atakayeajiri mtu asiye na sifa atalipa shillingi milioni mbili (2,000,000/=) fedha hizo zitalipwa Bodi ya korosho Tanzania baada ya kupewa taarifa ya maandishi na namba ya utambulisho ya malipo "control number". Faini hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Korosho ya mwaka 2009 kifungu cha 20 (3)(4)".

SEHEMU YA PILI

## 2.0. UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI NGAZI YA MKULIMA

### 2.1. Uvunaji Korosho Ghafi

2.1.1 Korosho inapaswa kukomaa ikiwa juu ya mti wa mkorosho na kabla ya Korosho kudondoka chini mkulima anapaswa kuhakikisha eneo la mzunguko wa matawi ya mkorosho ni safi.

2.1.2 Mkulima anapaswa kuokota Korosho zilizokomaa na kudondoka zenyewe na si kuchuma au kutikisa mti ili zidondoke.

2.1.3 Baada ya kuokota Korosho, mkulima anapaswa kutenganisha bibo na Korosho kwa kuizungusha Korosho mpaka inaachana na bibo. Endapo mkulima ana aina ya mikorosho ambayo vipande vya mabibo vinang'ang'ania na kubakia kwenye Korosho baada yakutenganishwa na mabibo, atapaswa kuviondoa vipande hivyo kwa kutumia kisu. Kazi hiyo ifanyike kwa uangalifu kuepuka kuitoboa Korosho kwenye sehemu ambayo bibo linajishika.

2.1.4 Mkulima anapaswa kuokota Korosho angalau mara 3 kwa wiki zinapoanza kudondoka na kuokota kila siku wakati korosho zinapokomaa kwa wingi na wakati wa mvua ili kuepuka kushuka kwa ubora.

### 2.2. Uanikaji wa Korosho Ghafi

2.2.1 Korosho zianikwe juani kwa muda wa siku 3-4 mfululizo zikigeuzwa. Ni vyema Korosho zianikwe katika sakafu nzuri, jamvi, mikeka au maturubai.

2.2.2 Korosho zianikwe hadi zikauke vizuri. Korosho zilizokauka vizuri zina sauti kali inayosikika "rattling sound" kama zitadondoshwa kwenye sakafu ya saruji au kuchezeshwa kwenye viganja.

2.2.3 Ili kujiridhisha na kiwango cha unyevu kifaa cha kupima unyevu kitumike na unyevu usizidi asilimia kumi (10%).

### 2.3. Uchambuaji (Sorting)

2.3.1 Mkulima anatakiwa kutenganisha korosho na vitu visivyo korosho kama vile mabaki ya mabibo makavu (kochoko), majani ya miti, mazao mengine,

kokoto, mawe au mchanga. Pia aondoe korosho zilizooza, korosho zisizokomaa, korosho ndogo sana na korosho zilizotoboka au kuanza kuota.

2.3.2 Mkulima akipeleka Korosho ambazo hazijachambuliwa na kukauka vizuri kwenye ghala la Chama cha Msingi atawajibika kwa gharama zozote zitakazohitajika kuboresha Korosho hizo.

2.3.3 Mkulima atakayegundulika kuruhusu, kusababisha au kuweka mchanga au kitu kisicho Korosho ilikuongeza uzito na kuchanganya korosho zisizo na ubora za misimu iliyopita kupeleka ghala la Chama cha Msingi atawajibika kwa mujibu wa sheria Na.18 ya mwaka 2009 kifungu cha 23(a) na Mwongozo huu.

## 2.4. Kuhifadhi Korosho Ghafi

2.4.1 Korosho zilizokauka na kuchambuliwa zihifadhiwe vizuri kabla ya kupelekwa ghalani.

2.4.2 Korosho inapaswa kuhifadhiwa sehemu kavu, isiyovuja na yenye hewa ya kutosha. Korosho zisipokaushwa vizuri zinaweza kuharibika, kuota au kuoza ndani ya muda mfupi wa uhifadhi.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0. UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI KATIKA NGAZI YA CHAMA CHA USHIRIKA CHA MSINGI

3.1 Karani wa AMCOS au mjumbe wa Bodi anayehusika na ubora anapaswa kukagua korosho za kila mkulima na kuhakikisha kwamba zimekauka, zimechambuliwa na hazijachanganywa na vitu visivyo korosho (mchanga, mawe, kochoko n.k) kabla ya kupokelewa katika ghala la Chama cha Msingi.

3.2 Vifaa vya ubora (kipima unyevu na mizani ndogo) vitumike kupima unyevu wa korosho na idadi ya korosho kwa kilo kabla hazijapokelewa ghalani. Aidha kila ghala la chama cha msingi kiwe na turubai kwaajili ya kuanika na kukagua korosho kabla ya kupokea.

3.3 Baada ya ukaguzi korosho zipimwe uzito na kuwekwa katika gunia la katani/kitani lenye alama za utambulisho wa chama husika kama zilivyoainishwa kwenye kiambatisho Na.1 na kuhifadhiwa ghala la chama cha Msingi.

3.4 Gunia za korosho zinapaswa kuhifadhiwa kwenye ghala lisilovuja, linaloruhusu mzunguko wa hewa na kupangwa juu ya chaga "pallet" ili kutunza ubora.

3.5 Gunia la kuhifadhi korosho linapaswa kuwa la katani/ kitani lenye ubora uliopitishwa na shirika la viwango Tanzania (TBS) lenye uwezo wa kuhifadhi kilo 80 za Korosho ghafi.

3.6 Wakati wa upakiaji wa Korosho watendaji wa Chama cha Msingi wanapaswa kujiridhisha na uzito na ubora wa korosho zinazopelekwa ghala la mnada na kuhakikisha uzito na ubora stahiki unafika ghalani.

3.7 Chama cha Ushirika cha Msingi kitakacho peleka korosho ambazo hazijakidhi Viwango kwenye ghala la mnada kama ilivyoainishwa katika kipengele cha 4.4.4 kwenye mwongozo huu, korosho hizo hazitaruhusiwa kutoka nje ya ghala hadi itakapothibitika ufinyu wa nafasi katika ghala husika. Chama cha Msingi kitawajibika kwa gharama zote zitakazohitajika kuboresha korosho hizo.

3.8 Viongozi/Watendaji wa Chama cha Ushirika cha Msingi watakaobainika kuchanganya korosho na vitu visivyo korosho au korosho zisizokidhi viwango vya ubora ili kuongeza uzito na kupeleka ghala la mnada watawajibika kwa mujibu wa kifungu cha 23(a) cha sheria Na. 18 ya Tasnia ya Korosho.

## SEHEMU YA NNE

# 4.0. UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI KATIKA GHALA LA MNADA

## 4.1. Taratibu za Kuingiza Korosho Ghala la mnada

4.1.1 Korosho zitakazopelekwa kwenye ghala la mnada zitahakikiwa na kuthibitishwa ubora kulingana na viwango vilivyoainishwa katika mwongozo huu na Mwongozo wa pamoja wa mauzo msimu wa korosho wa mwaka 2025/2026.

4.1.2 Vitabu vya Hati ya Ubora vinavyotolewa na Bodi ya korosho vitatolewa kwa namba maalum (serial number) kwa ghala husika. Haitaruhusiwa kubadilishana vitabu vya ubora kutoka ghala moja na lingine wala haitaruhusiwa kutumia vitabu vya msimu uliopita. Vitabu vyote vilivyotumika na vipya virudishwe Bodi ya korosho baada ya msimu kuisha. Kitabu kimoja cha Hati za Ubora kitalipiwa kwa sh.25,000/=.

4.1.3 Korosho zitapokelewa katika ghala la mnada kwa madaraja yote mawili "daraja la kwanza na daraja la pili" wakati wote wa msimu' Korosho daraja la kwanza na daraja la pili zipangwe katika loti tofauti.

4.1.4 Aidha upangaji wa Korosho ghafi katika ghala utazingatia loti/stake zenye SHOT 50lbs/80kg - nakuendelea, loti/stake ya 48lbs/80kg na 49lbs/kg na loti/stake zenye SHOT 44lbs/80kg - 47lbs/kg bila kuathiri Madaraja yanayotambulika kisheria.

4.1.5 Korosho ghafi ambazo hazijakidhi viwango vya ubora kama ilivyoainishwa katika kipengele cha 4.4.4 katika mwongozo huu, viongozi wa AMCOS washauriwe kuboresha korosho hizo ghalani ili kufikia vigezo vya ubora. Korosho ambazo hazitakidhi zihifadhiwe katika ghala kwa makubaliano maalumu na itolewe stakabadhi ya korosho mbovu zinazo baki ghalani. Baada ya msimu kukamilika (korosho zitahakikiwa na Bodi ya korosho na zitakazokuwa na SHOT ya 35lbs/80kg zitaruhusiwa kubanguliwa ndani ya nchi chini ya hapo zitaondolewa kwenye mzunguko kwa makubaliano ili kulinda soko la msimu ujao.

4.1.6 Taratibu zote za kuhakiki ubora wa korosho zinazopokelewa kwenye ghala la mnada utafanywa na mtaalam wa mwendesha ghala mbele ya mwakilishi wa AMCOS na kuweka kumbukumbu katika kitabu cha hati ya Ubora kinachotolewa na Bodi ya korosho Tanzania kwa mujibu wa taratibu za kupokea korosho kwenye ghala la mnada.

4.1.7 Vyama Vikuu vya Ushirika vina wajibu wa kuajiri wataalamu wa ubora waliopata mafunzo na cheti cha uhakiki ubora kutoka Bodi ya Korosho watakaosimama kwa niaba ya wakulima katika ghala la mnada kuhakikisha kuwa upimaji ubora wa korosho zinazopokelewa unafanyika kwa kuzingatia taratibu zote za uhakiki ubora.

## 4.2. Utaratibu wa Kuchukua Sampuli

4.2.1 Hatua ya msingi katika zoezi la uhakiki ubora wa Korosho ghafi ni jinsi ya upatikanaji wa sampuli. Mtaalamu wa ubora anapaswa kuzingatia hatua zifuatazo wakati wa uchukuaji wa sampuli.

4.2.2 Sampuli itolewe kwa uangalifu kwa kutumia sampuli nasibu "random sampling" kutoka katika mzigo wa Korosho ghafi.

4.2.3 Kifaa maalum cha kuchukulia sampuli kitatumika kuchukua sampuli kutoka pande zote nne na katikati kwa kila gari litakalopeleka mzigo ghala la mnada.

4.2.4 Sampuli inapaswa iwe ya kweli na iliyochukuliwa kutoka katika gari husika (representative sample).

4.2.5 Sampuli inapaswa kuchukuliwa zaidi ya asilimia 60% ya magunia yote yaliyo kwenye gari. Kadri sampuli inavyokuwa kubwa na usahihi wa matokeo unaongezeka.

4.2.6 Iwapo mtaalamu wa uhakiki ubora atagundua kasoro au kuwa na wasiwasi wowote kuhusu ubora wa mzigo uliobebwa kwenye gari husika anapaswa kuchukua sampuli ya mzigo wote (100%) ili kujiridhisha na usahihi wa uhakiki ubora atakaofanya. Iwapo itagundulika kuna kitu chochote kisicho korosho kama mchanga, mawe, kuchoko (mabibo makavu) na vinginevyo, korosho zote zishushwe na

kukaguliwa na taarifa itolewe kwa Bodi ya Korosho na mamlaka nyingine katika eneo husika.

4.2.7 Iwapo itagundulika kuna unyevu wa kiwango cha juu kwenye magunia yaliyofungasha korosho, gari zima likaguliwe na magunia yatakayobainika kuwa na changamoto ya unyevu yashushwe na korosho zianikwe na kuchambuliwa ili zikidhi vigezo vya ubora kabla ya kupokelewa ghalani kwa mujibu wa mwongozo huu.

4.2.8 Sampuli itakayochukuliwa ili kuhakiki ubora inatakiwa iwe na unyevu usiozidi asilimia kumi (10%) ili mzigo upokelewe ghalani.

4.2.9 Sampuli ichanganywe vizuri kisha ipimwe na wastani wa sampuli katika zoezi la uhakiki ubora wa korosho ghafi "cutting test" ni kilo moja.

## 4.3. Vifaa Vinavyohitajika Katika Zoezi la Uhakiki Ubora

i. Kipima unyevu (moisture meter) kilichofanyiwa ugezi "calibration" na "TBS"
ii. Mkasi wa kukatia Korosho
iii. Bisibisi au kichoteo (scooper)
iv. Mizani ndogo ya kidijitali ithibitishwe na (WMA)
v. Kifaa maalum cha kuchukulia sampuli
vi. Kikokotoo (calculator), kalamu na daftari dogo
vii. Mafuta ya nazi au nyonyo au "gloves"
viii. Bakuli au sahani zenye rangi tofauti
ix. Tishu au kitambaa maalumu
x. Meza ya kukatia sampuli
xi. Chombo cha kubebea sampuli (ndoo au gunia)
xii. Hati ya Ubora kutoka Bodi ya korosho.

## 4.4. Taratibu za Kupima Sampuli

Mtaalamu wa ubora anapaswa kufuata taratibu zifuatazo wakati wa kupima sampuli ya korosho ghafi.

4.4.1 Sampuli ipimwe asilimia ya unyevu "moisture content" kwa kutumia kifaa maalumu kiitwacho kipima unyevu "moisturemeter" kilichofanyiwa ugezi

"Calibration" na shirika la Viwango Tanzania (TBS) na asilimia ya unyevu izingatie "correction factor" ya kifaa husika. Kiwango cha unyevu kinapaswa kisizidi asilimia kumi 10% (w/w).

4.4.2 Sampuli ipimwe kilo moja na kuhesabiwa idadi ya korosho kwa kilo (nut count). Kipimo hiki hutegemea ukubwa na uzito wa Korosho katika kilo moja na idadi ya Korosho haipaswi kuzidi mia mbili (200) kwa kilo.

4.4.3 Korosho zilizohesabiwa zikatwe kwa kutumia mkasi maalum wa kukatia korosho ghafi kisha ziwekwe mafungu tofauti kwa Korosho zilizokatwa kama ifuatavyo:

GN - "Good kernels" (Korosho karanga nzuri)

IMM - "Immature kernels" (Korosho karanga zisizokomaa)

SP - "spotted kernels" (Korosho karanga zenye madoa)

RT - Rotten (Korosho zilizooza)

VD - Void (Korosho zisizokuwa na kitu ndani)

Kisha njia ifuatayo itumike kutafuta "shelling out Turn"

$$SHOT = \left(GN + \frac{(IMM + SP + PD)}{2}\right) \times 0.176$$

4.4.4 Madaraja ya Korosho ghafi yanayotambulika kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 ya mwaka 2009 na kanuni ya 26 ya kanuni za Tasnia ya Korosho za mwaka 2010, ni daraja la kwanza na daraja la pili.

**Daraja la kwanza**

SHOT = 48lbs/80kg bag na zaidi(>48lbs/80kgbag).

Unyevu wa Korosho "Moisture content" usizidi asilimia kumi 10% (w/w).

Idadi ya Korosho kwa kilo moja "Nut count" inapaswa isizidi mia mbili (200).

**Daraja la Pili**

SHOT =(44lbs/80kg bag - 47 lbs/80kg bag).

Unyevu wa Korosho "Moisture content" usizidi asilimia kumi 10% (w/w).

Idadi ya Korosho kwa kilo moja "Nut count" inapaswa isizidi mia mbili (200).

4.4.5 Korosho zenye ukungu kwa nje aidha wa rangi nyeupe, kijani, nyeusi au njano zisipokelewe kwenye ghala la korosho kuanzia ngazi ya AMCOS hadi ghala kuu, wakulima wazingatie kutenganisha vizuri korosho na bibo na kukausha korosho vizuri kuepuka changamoto hii.

4.4.6 Mtaalamu wa ubora wa ghala la mnada atakapo bainika kukiuka taratibu za uhakiki ubora zilizoainishwa kwenye mwongozo huu na kusababisha uwepo wa Korosho zisizokidhi viwango ghalani au kutoa taarifa zisizosahihi kuhusu kiwango cha ubora. Mtaalamu huyo atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa leseni ya uhakiki ubora kutoruhusiwa kusimamia ubora katika ghala za mnada kwa kipindi cha misimu mitatu mfululizo.

## 4.5. Taratibu za Kutoa Korosho Ghala la Mnada.

4.5.1 Kabla ya mnada timu maalum itahakiki ubora wa korosho ghafi na kutoa taarifa kwaajili ya kuendelea na mnada.

4.5.2 Mnunuzi anawajibika kuhakiki ubora wa korosho alizonunua mnadani na kulipia kabla ya kuzitoa katika ghala la mnada kwa kufuata taratibu zilizoainishwa katika mwongozo huu. Mtaalamu wa ubora wa mwendesha ghala ni mhusika mkuu na mtaalamu wa ubora wa mnunuzi ni shahidi.

4.5.3 Mnunuzi anaruhusiwa kuwa na mtaalamu wa ubora aliyepitia mafunzo ya uhakiki Ubora wa Korosho ghafi msimu wa 2025/2026 yaliyotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania, atakayemuwakilisha katika ghala la

mnada wakati wa uhakiki wa ubora wa Korosho ghafi kabla ya kuzitoa ghala la mnada.

4.5.4 Mnunuzi atapewa korosho kwenye ghala la mnada kwa kuzingatia daraja la korosho alizonunua mnadani. Fomu maalumu inayoonyesha ubora wa korosho alizochukua iandaliwe na Mwendesha ghala husika, Mnunuzi apewe nakala halisi na Mwendesha ghala abaki na nakala.

4.5.5 Mwendesha ghala atakayetoa taarifa za uongo za ubora na ikadhibitika utofauti ya daraja la ubora wa korosho, unyevu wa korosho na idadi ya korosho kwa kilo kwa korosho zilizohifadhiwa katika ghala la mnada wakati wa ukaguzi utakaofanywa na Bodi ya Korosho, barua ya malalamiko ya ubora kutoka kwa mnunuzi aliyenunua korosho hizo mnadani au kamati ya uhakiki ubora. Mwendesha ghala atawajibika kuboresha na kuhakikisha mnunuzi anapata kiwango cha ubora na uzito alionunua au kumlipa mnunuzi utofauti wa bei kwa kuzingatia ubora. Aidha Itakapothibitika ubora wa korosho zilizohifadhiwa ghalani umeshuka Mwendesha ghala atawajibika kulipa Bodi ya korosho adhabu ya Shillingi milioni tano (5,000,000/=) kwa kila kosa la ubora litakalothibitika.

4.5.6 Mnunuzi yoyote atakayeshiriki na kuthibitika kuchangia kushuka kwa ubora baada yakukabidhiwa Korosho katika ghala la mnada au kuongeza kitu chochote ambacho sio Korosho atawajibika kwa mujibu wa kifungu cha 23(b) cha Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya mwaka 2009.

### 4.6. Sifa za Ghala la Kuhifadhia Korosho

i. Ghala linapaswa kuwa na milango angalau pande mbili za kuta na madirisha madogo "vents" za kutosha juu na chini kurahisisha mzunguko wa hewa ghalani.

ii. Ghala liwe na chaga "pallets" za kuwekea korosho ghafi'

iii. Ghala liwe na sakafu ya saruji iliyo safi.

iv. Ghala halipaswi kuvuja au kuingiza maji wakati wa mvua.

v. Ghala liwe na vifaa vyote vya ubora kama vilivyotajwa katika kipengele 4.3 vinavyofanyakazi vizuri na vilivyoidhinishwa na mamlaka husika na kuthibitishwa na Bodi ya Korosho.

vi. Ghala linapaswa kuwa na sifa zote kama zinavyoelekezwa na Bodi ya Stakabadhi za Ghala.

### 4.7. Ghala kuu litapangiliwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:

i. Kwa kutumia rangi ya njano au nyeupe, kuchora mipaka ya eneo la fungu la korosho na njia ya kupita katika sakafu ya ghala lote na kulipa namba kwa kila eneo;

ii. Kuacha nafasi (njia) yenye upana wa **mita 1** kutoka ukuta wa jengo kwa kila upande wa ghala ;

**iii.** Kuacha nafasi (njia) ya kati yenye upana wa **mita 2** kati ya fungu moja na lingine. Kwa ruhusa maalum kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, nafasi hii inaweza kupungua hadi kufika **mita 1;**

iv. Kimo cha fungu la korosho hakitakiwi kuzidi safu (tabaka) 18. Kwa ruhusa maalum kutoka Bodi, safu zinaweza kuongezeka hadi kufika safu 22. NB: Takaba ya juu haitakiwi kuziba dirisha la hewa (vent)

v. Nafasi juu ya fungu haitapungua **mita 2** kutoka kwenye ncha ya chini ya paa la jengo la ghala.

vi. Steka za korosho zitapangwa kwa kuzingatia kifungu 4.1.4 cha Muongozo huu.

### 4.8. Udhibiti Ubora wa Korosho Ghafi Ngazi ya Msafirishaji

4.8.1 Msafirishaji anawajibika kuwa na nyaraka zote zinazotambulika kisheria za gari husika linalotumika kubeba korosho ghafi katika msimu 2025/2026.

4.8.2 Msafirishaji anawajibika kuwa amesajiliwa na Bodi ya Korosho Tanzania.

4.8.3 Msafirishaji akishakabidhiwa korosho ghafi katika ghala la mnada atawajibika kulinda na kutunza ubora na uzito wa korosho hizo hadi kwenye ghala la mnunuzi, bandarini au kiwandani.

4.8.4 Msafirishaji /mmiliki wa gari au chombo chochote cha usafiri atakayebainika kusafirisha korosho mbovu kwa kujua au kwa kutokujua atatozwa faini ya kiasi cha shillingi million moja na laki tano (1,500,000) na mwenye mzigo atatozwa faini ya shillingi million moja na laki tano (1,500,000) na mzigo huo utataifishwa na kuondolewa kwenye mzunguko kwa gharama za mwenye mzigo.

4.8.5 Msafirishaji yoyote atakayeshiriki na kuthibitika kuchangia kushuka kwa ubora baada ya kukabidhiwa korosho kutoka ghala la chama cha msingi au ghala la mnada au kuongeza kitu chochote ambacho sio korosho atawajibika kwa mujibu wa Sheria za nchi.

## SEHEMU YA TANO

# 5.0. MAJUKUMU NA WAJIBU WA WADAU KATIKA KUSIMAMIA UBORA WAKOROSHO GHAFI

## 5.1. Mkulima

i. Kuzingatia taratibu zote za uvunaji, ukaushaji, uchambuaji/udarajishaji na uhifadhi wa korosho ghafi katika madaraja kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya pili ya Mwongozo huu.

ii. Kupeleka Korosho kwenye ghala la AMCOS, kuhakikisha korosho zake zimekaguliwa kwa kumwaga korosho zote mbele ya mjumbe anayesimamia ubora.

iii. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

## 5.2. Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS)

i. Kuajiri karani wa ubora au kuwa na mjumbe wa AMCOS atakayesimamia ubora wa korosho katika kila ghala la Chama cha Ushirika cha Msingi.

ii. Kuhakikisha ghala linalotumika kupokelea korosho kutoka kwa wakulima lipo katika hali nzuri na halivuji.

iii. Kuhakikisha magunia yote yameandikwa au yamechapishwa alama za utambulisho kama zilivyoainishwa kwenye kiambatisho Na.1 kabla ya kusafirishwa kwenda ghala la mnada.

iv. Mjumbe wa Bodi au Mtendaji wa Chama cha Msingi husika ahakikishe korosho ghafi anazifanyia ukaguzi wa awali wa ubora kabla ya kusafirisha kwenda ghala la mnada.

v. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

### 5.3. Vyama Vikuu vya Ushirika

i. Kuajiri Mtaaamu wa ubora atakayetoa elimu kwa Vyama vya Msingi na kusimamia mapokezi ya korosho ghala la mnada.
ii. Kwa kushirikiana na Bodi ya korosho pamoja na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kuhakikisha ghala zinazopewa leseni ya kuhifadhi Korosho linakidhi viwango vyote vya kuhifadhi Korosho ghafi.
iii. Kwa kushirikiana na Bodi ya korosho na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kuhakiki na kupata kampuni za waendesha ghala zenye sifa katika zao la korosho.
iv. Kwa kushirikiana na Bodi ya korosho na Bodi ya Usimamzi wa Stakabadhi za Ghala kusimamia utekelezaji wa shughuli zote kwenye ghala la mnada.
v. Kununu ana kusambaza gunia za katani/kitani zenye ubora na uzito uliothibitishwa na TBS kwa wakati.

### 5.4. Mtaalam wa Ubora ghala la mnada

i. Kuhakiki ubora wa Korosho ghafi kabla hazijapokelewa ghalani kwa kuzingatia Mwongozo Na.2 wa Usimamizi wa Udhibiti Ubora wa Korosho Ghafi wa mwaka 2025/2026.
ii. Kuhakikisha korosho ghafi zinapangwa kwa kuzingatia madaraja yaliyoainishwa kwenye Mwongozo huu.
iii. Kuomba na kufuatilia leseni ya kufanya kazi ya uhakiki ubora kwa mwaka husika kutoka Bodi ya Korosho Tanzania.
iv. Mtaalam wa Ubora yeyote atakayethibitika kushindwa kuteleza majukumu yake na kusababibisha kuingiza ghalani korosho ambazo hazijakidhi viwango vya ubora kwa mujibu wa kifungu cha 4.4.4 atawajibika kwa kuzingatia kipengele 4.4.6 cha Mwongozo huu.

### 5.5. Mwendesha Ghala

i. Mwendesha ghala anapaswa kuwa na vifaa vya ubora kama vilivyoainishwa katika kipengele 4.3 na viwe vimehakikiwa na mamlaka husika (TBS na WMA). Vifaa vyote viwepo ghala la

mnada kabla ya zoezi la kupokea Korosho kuanza. Iwapo mwendesha ghala atathibitika kuwa na vifaa pungufu au havijahakikiwa na mamlaka husika. Mwendesha ghala atawajibika kulipa Bodi ya korosho faini ya shillingi million moja (1,000,000/=).

ii. Mwendesha ghala lazima awe na wataalamu wa ubora wa Korosho angalau wawili waliosajiliwa na kupata kibali toka Bodi ya Korosho.

iii. Mwendesha ghala ana wajibu wa kutoa taarifa ya maandishi Bodi ya Korosho endapo kutatokea ulazima wa kubadilisha mtaalamu wa ubora wakati msimu ukiwa unaendelea.

iv. Mwendesha ghala ahakikishe ghala lake lina sifa zilizotajwa katika kipengele 4.6 na limepangwa kwa kuzingatia kipengele 4.7 cha mwongozo huu.

v. Mwendesha ghala atawajibika kukagua magunia ya korosho anayopokea kwenye ghala la mnada na kuhakikisha yana alama za utambulisho kama zilivyoainishwa kwenye kiambatisho Na.1.

vi. Mwendesha ghala anapaswa kupokea korosho zenye ubora unaotambulika na sheria ya tasnia ya Korosho kama ilivyoelezwa katika kipengele 4.4.4.

vii. Kutunza Korosho za wakulima na kutoa korosho kwa wanunuzi kuzingatia daraja la ubora alilonunua kwenye mnada na kwa kuzingatia mwongozo huu.

viii. Kuzingatia korosho zinazoingia awali ghalani ndizo zitakazotoka mwanzo "First in First out" (FIFO) wakatiwa kutoa korosho katika ghala la mnada.

ix. Kuhakikisha mnunuzi anahakiki ubora kabla ya kuchukua Korosho kwenye ghala la mnada na kusaini kuwa amechukua Korosho zenye ubora kama ilivyobainishwa kwenye stakabadhi husika.

x. Kuhakikisha wataalamu wa ubora ghalani maslahi yao yanazingatiwa kwa mujibu wa maelekezo wa Bodi ya Usimamizi wa stakabadhi za Ghala.

xi. Iwapo kutatokea malalamiko ya ubora kutoka kwa mnunuzi Mwendesha ghala atagharamia shughuli yote ya ubora itakayofanywa na timu ya ubora itakayoundwa kwa zoezi hilo.

xii. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

## 5.6. Wanunuzi wa Korosho Ghafi

i. Kuhakiki ubora wa Korosho alizonunua kabla ya kutoa ghala la mnada. Endapo, pande zote mbili (Mwendesha Ghala na Mnunuzi) hawatakubalia na utaratibu wa kupima au matokeo ya ubora, anayepinga atatakiwa kuwasilisha malalamiko yake kwa maandishi Bodi ya KoroshoTanzania.

ii. Mnunuzi akitoa korosho ghala la mnada atawajibika kusimamia usafirishaji wa Korosho hizo na kuhakikisha analinda na kutunza uzito na ubora wa Korosho alizotoa katika ghala la mnada.

iii. Mnunuzi atawajibika kuhakikisha Korosho zinasafirishwa zikiwa na magunia yenye alama za utambulisho kama zilizoainishwa kwenye kiambatisho Na.1, ili kurahisisha mfumo wa ufuatiliaji "traceability". Endapo atahitaji magunia ya ziada atalazimika kununua kutoka chama Kikuu cha Ushirika.

iv. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

## 5.7. Wasafirishaji wa Korosho Ghafi

i. Msafirishaji anatakiwa kuhakikisha anasafirisha korosho katika hali ya usalama bila kuharibu ubora wa korosho hizo.

ii. Msafirishaji ghala la mnada hadi ghala la mnunuzi /bandarini anapaswa kujisajili Bodi ya Korosho.

iii. Msafirishaji anatakiwa kuhakikisha korosho hazinyeshewi na mvua katika muda wote wa safari.

iv. Mwakilishi wa chama na msafirishaji wanatakiwa kufikisha Korosho kwenye ghala la mnada katika uzito na ubora waliopokea kutoka ghala la chama cha Msingi husika.
v. Mwakilishi wa mnunuzi au msafirishaji anatakiwa kufikisha korosho bandarini au ghala la mnunuzi katika uzito na ubora waliopokea kutoka ghala la mnada.
vi. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

**5.8. Halmashauri**

i. Maafisa kilimo wa kata na kijiji husika na maafisa BBT wanatakiwa kutoa elimu ya uvunaji, ukaushaji, uchambuaji na uhifadhi wa korosho kwa wakulima wa eneo husika ili kuzingatia ubora katika ngazi ya mkulima.
ii. Maafisa kilimo/ugani wa kata na maafisa kilimo BBT wanatakiwa kufanya ukaguzi kwenye ghala za AMCOS kuhakiki kama ukaguzi wa awali wa korosho za wakulima unafanyika kwa kuzingatia Mwongozo huu.
iii. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

**5.9. Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA)**

i. Kukagua na kuthibitisha mizani itakayotumika kupima Korosho.
ii. Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kusuluhisha migogoro inayotokana na vipimo.

**5.10. Bodi ya Usimamiziwa Stakabadhi za Ghala**

i. Kwa kushirikiana na Bodi ya korosho pamoja na Vyama Vikuu vya Ushirika kuhakikisha ghala zinazopewa leseni ya kuhifadhi Korosho linakidhi viwango vyote vya kuhifadhi Korosho ghafi.
ii. Kwa kushirikiana na Bodi ya korosho na Vyama vya Vikuu vya Ushirika kuhakiki na kupata kampuni za waendesha ghala zenye sifa katika zao la korosho.

iii. Kwa kushirikiana na Bodi ya korosho na Vyama Vikuu vya Ushirika kusimamia utekelezaji wa shughuli zote kwenye ghala la mnada.
iv. Kusimamia utekelezajiwa sheria na kanuni ya stakabadhi za ghala.
v. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

### 5.11. Bodi ya Korosho Tanzania

i. Kufanya ukaguzi wa vifaa vya ubora kabla na wakati wa msimu.
ii. Kufanya ukaguzi wa ghala za minada na shughuli nyingine za utendaji wa mwendesha ghala kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala pamoja na Vyama Vikuu vya Ushirika.
iii. Kuratibu na kutoa mafunzo ya ubora kuanzia ngazi ya mkulima, viongozi wa AMCOS na wataalamu wa uhakiki ubora wa korosho ghafi katika ghala la mnada.
iv. Kutoa vitabu vya hati ya uhakiki ubora wa korosho kwa mwendesha ghala.
v. Kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika ghala za vyama vya msingi kwa kushirikiana na Maafisa ushirika wa Wilaya husika na ukaguzi ghala za mnada kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Vyama Vikuu vya Ushirika ili kuhakikisha sheria na taratibu za ubora zinafuatwa.
vi. Kutatua migogoro ya ubora pale inapotokea katika mnyororo wa mauzo.

## SEHEMU YA SITA

### 6.0. UTATUZI WA MIGOGORO

6.1 Changamoto ya ubora itakapotokea katika ghala la mnada taarifa ya maandishi itumwe Bodi ya Korosho ndani ya saa 48 tangu kutokea changamoto na Bodi itashirikiana na Bodi ya Usimamizi wa ghala kutatua changamoto zinazomuhusu mwendesha ghala. Aidha Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania anaweza kuunda timu maalum kutoka katika taasisi mbalimbali kama atakavyoona inafaa kutatua changamoto husika.

6.2 Bodi ya Korosho itashughulikia changamoto hiyo kwa mujibu wa Kifungu cha 3 (e) cha sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya mwaka 2009 na kutoa maamuzi.

***Mwongozo huu unatakiwa kusomwa sambamba na sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya mwaka 2009 (Tangazo la serikali Na. 420 la mwaka 2010). Pamoja na Mwongozo namba 1 wa Masoko na Mauzo ya korosho msimu wa 2025/2026. Atakayekiuka matakwa ya mwongozo huu atakuwa anatenda kosa hivyo atachukuliwa hatua kwa muiibu wa sheria.***

***Mwongozo huu umetolewa** 15 Septemba **2025***

Francis Alfred

**MKURUGENZI MKUU**

*Kiambatisho Na.1*

**RANGI NA ALAMA ZA MAGUNIA YA KOROSHO GHAFI MSIMU WA 2025/2026**

| S/N | Jina la Chama Kikuu | Rangi ya Majina ya Utambuzi | MKOA | Jina kwa kila gunia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | TANECU Limited | Nyekundu | Mtwara | MTW/TANECU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 2. | MAMCU Limited | Blue | Mtwara | MTW/MAMCU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 3. | RUNALI Limited | Zambarau | Lindi | LND/RUNALI/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 4. | LINDI MWAMBAO Limited | Njano | Lindi | LND/LINDI MWAMBAO/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 5. | TAMCU Limited | Nyeusi | Ruvuma | TNDR/ TAMCU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 6. | CORECU Limited | Kijani | Pwani | PWN/CORECU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 7. | TACACU Limited | Nyeupe | Tanga | TNG/TACACU/Na. ya usajili wa Chama cha Msingi |
| 8. | CEAMCU Limited | Waridi | Singida | CEAMCU/ Na. ya Usajili wa Chama cha Msingi. |
| 9. | DOMASICA Limited | Chokleti | Dodoma | DOMACICA/Na.ya Usajili Chama cha Msingi |
| 10. | UKICU Limited | Machungwa | Morogoro | UKICU/Na.ya Usajili wa Chama cha Msingi. |
| 11. | KICU | Machungwa | Morogoro | KICU/Na.ya Usajili wa Chama cha Msingi. |
| 12 | MOFACU | Machungwa | Morogoro | MOFACU/Na. ya Usajili wa Chama cha Msingi. |

NB: ***Magunia yote yataandikwa:-Cashewnut Produce of Tanzania***